

**RISALA YA MH WAZIRI WA NCHI OMKR, MKESHA WA  
KUAMKIA SIKU YA UKIMWI DUNIANI,2021**

**Ndugu Wananchi,**

Kama tunavyofahamu kwama ifikapo tarehe 1 Disemba, Dunia huadhimisha siku ya **UKIMWI**. Hapa Zanzibar tokea mwaka 1988 tumekuwa tukiadhimisha siku hii lengo likiwa ni kujitathmini katika jitihada zetu za kupambana na maradhi haya, kuwafaraji wenzetu ambao wanaishi na Virusi vya UKIMWI pamoja na kuwakumbuka wale ambao wamefariki kutokana na maradhi haya thakili.

Katika kuadhimisha siku hii, kila mwaka huwepo na kauli mbiu, na kauli mbiu ya mwaka huu wa 2021 ni **“TUWEKE USAWA KUMALIZA UKIMWI NA MAJANGA MENGINE”**. ikiwa ni msisitizo katika kuweka usawa wa upatikanaji wa huduma za VVU na UKIMWI kwa watu wote.

Kukosekana kwa usawa katika upatikanaji wa huduma za VVU na UKIMWI kunachangia kuendelea kuwepo kwa maradhi ya UKIMWI na watu kupata maambukizo mapya ya VVU.

**Ndugu Wananchi,**

Ingawa Zanzibar tumefanikiwa kwa kiwango kikubwa kufikia malengo ya kudhibiti UKIMWI, uchambuzi wa takwimu mbali mbali unaonesha kwamba bado kuna baadhi ya makundi hayajaweza kufikiwa ipasavyo na huduma zinazotolewa. Kwa mfano wanawake wanaonekana kufanya vizuri katika kuzifikia na kuzitumia huduma kama vile za ushauri nasaha na upimaji wa VVU, huduma za

matumizi ya dawa za kupunguza makali ya Virusi (ARV) na kupunguza kiwango cha Virusi vya UKIMWI mwilini.

Katika watu **166,566** waliopatiwa huduma ya ushauri nasaha na uchungzi wa VVU baina ya Januari hadi Septemba mwaka huu wengi wao walikuwa ni wanawake ambao ni 86,947 ukilinganisha 79,619 ya wanaume. Aidha katika watu 7,481 wanaotumia dawa za ARVs hadi kufikia Sepetemba mwaka huu, 5,170 ni wanaake ukilinganisha na 2,427 ya wanaume. Tofauti hizi zina athari kubwa katika kudhibiti maambukizo ya VVU na kumaliza janga la UKIMWI.

### **Ndugu Wananchi**

Wakati tukiendelea na juhudi za kupambana na maradhi ya UKIMWI na hatimaye tulimalize kabisa ifikapo 2030, eneo jengine ambalo limekuwa likizorotesha juhudi zetu ni suala la unyanyapaa. Bado kiwango cha unyanyapaa katika jamii yetu kipo juu. Asilimia 30 ya watu Wazanzibari wamekuwa na tabia za unyanyapaa kwa watu wanaoishi na VVU. Hali hii inachangia kuwafanya watu kuzikimbia huduma za upimaji wa VVU, kuficha hali zao za maambukizo na kuongeza uwezekano wa maambukizo mapya katika jamii.

### **Ndugu Wananchi,**

Nichukuwe fursa hii niendeleo kuwakumbusha kwamba UKIMWI bado ni janga la kitaifa. Hatuna budi tushirikiane kwa kujiepusha na mambo yanayochangia maambukizo mapya katika jamii. Aidha nichukuwe fursa hii kuwaomba kushiriki kwa wingi katika kilele cha maadhimisho ya siku ya UKIMWI ambayo Kitaifa yatafanyika

Kidimni, Wilaya ya Kati siku ya tarehe 1 Jumatano asubuhi. Mgeni Rasmi katika maadhimisho hayo anatarajiwa kuwa Mh. Makamo wa Kwanza wa Rais, Mh Othman Masoud. Shime tujitokeze kwa wingi

Ahsanteni kwa kunisikiliza